AGENDA

For Environment and Responsible Development

**Kwa vyombo vya habari: 30/06/2017**

## Utafiti mpya wa rangi wabaini kupungua kidogo kwa kiwango cha madini ya risasi kwenye rangi za kupamba, hata hivyo bado baadhi ya rangi zina viwango vikubwa vya madini hayo

### *Vifungashio vya rangi bado havina taarifa kuhusu viwango vya madini ya risasi hivyo kuwa vigumu kwa watumiaji kuchagua rangi salama kwenye soko*

**(Dar es Salam, Tanzania)** Taasisi ya AGENDA *for Environment and Responsible Development* (AGENDA) leo inatoa taarifa kufuatia utafiti iliyofanya ikihusisha aina 46 za rangi za mafuta (Solvent) kwa matumizi ya kupamba nchini. Utafiti huu unalinganisha utafiti uliofanyika mwaka 2015 na unaonesha mabadiliko kidogo kulingana na utafiti wa awali, ingawa baadhi ya rangi bado zimeonekana kuwa na viwango vikubwa vya madini hayo. Taarifa ya utafiti huu ni moja ya taarifa ya tafiti kama hizi katika ya nchi nyingine nne za Afrika kupitia mpango wa Mradi wa Kuondoa Madini ya Risasi Kwenye Rangi Barani Afrika (African Lead Paint Elimination Project).

Matokeo ya utafiti huu mpya yanaonesha asilimia 46 ya rangi zilizohusishwa (21 kati ya rangi 46) kuwa na kiwango cha madini ya risasi zaidi ya sehemu 90 ya milioni(parts per million - ppm) ukilinganisha na asilimia 64 kwa utafiti wa mwaka 2015. Kiwango cha sehemu 90 ya milioni ndicho kilichopitishwa na wawakilishi wa nchi zaidi ya 20 za Afrika kama kiwango cha ukomo kisheria. Pia ni kiwango ukomo kisheria kwa nchi za India na Marekani.

Moja u zaidi ya rangi zinazouzwa, 7 kati ya chapa 12 za rangi zinazouzwa zaidi nchini zilizohusishwa katika utafiti huu zimeonekana kuwa na viwango vikubwa vya madini ya risasi ambayo ni zaidi ya kipimo cha vipande 10,000 kwa vipande milioni moja. Rangi za kampuni hizi ni zile zinazozalishwa nchini na zinazonunuliwa toka nje ya nchi. Kiwango cha juu kabisa cha madini ya risasi kinaripotiwa kufikia vipande 84,000 kati ya vipande milioni moja katika moja ya rangi za njano na kijani, zote zikiwa ziliagizwa toka nje ya nchi na kuuzwa nchini. Pia, ingawa kuna rangi zenye viwango salama vya madini ya risasi katika soko nchini, wanunuzi hawana njia bora ya kuweza kupapambanua rangi salama na zisizo salama kutokana na kukosekana viwango ashiria vya madini ya risasi katika vifungashio (labels) vya rangi kwa sasa. Shirika la viwango Tanzania (TBS) iko kwenye mchakato wa kupitisha viwango vya madini ya risasi nchini ambapo itasaidia kupunguza tatizo hili ikipitishwa na kusimamiwa utekelezaji wake.

“Athari za madini ya risasi kwa ubongo wa watoto ni umri wao wote, hayarekebishiki wala hayatibiki,” alisema Prof. Jamidu Katika, Mwenyekiti wa AGENDA. “ Ni azima kupunguza chanzo hiki kikuu cha madini ya risasi yasiweze kuathiri watoto wetu. TBS inashauriwa kumaliza mapema iwezekanavyo na kuisimamia viwango vya madini ya risasi kwenye rangi zinazozalishwa nchini, zinazoagizwa nje, zinazouzwa na zinazotumika pamoja na bidhaa zinazopakwa nayo. Hii ni muhimu ili kulinda afya za watoto wetu.

Mwaka 2017, AGENDA ilinunua makasha 46 ya rangi za mafuta za kupaka kwenye nyumba kutoka mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Mwanza. Rangi hizo ni za chapa 12 zinazozalishwa nchini na zinazoagizwa toka nje. Sampuli zote za Tanzania na kutoka nchi nyingine 3 za Afrika zilipelekwa katika maabara iliyothibitishwa kitaalamu iliyopo nchini Marekani (USA) ili

kutathmini kiwango cha jumla cha uzito wa rangi kavu cha madini ya risasi. Matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:

- Chini ya nusu ya idadi za rangi zilizofanyiwa tathmini (21 kati ya rangi 46) zilionekana kuwa na madini ya risasi zaidi ya vipande 90 kati ya vipande milioni moja.
- Kumi kati ya rangi 46 (22%) zilionekana kuvuka kiwango cha juu zaidi, zaidi ya vipande 10,000 kati ya vipande milioni moja.
- Rangi za njano na nyekundu zilionekana kuwa na viwango vya juu zaidi vya mamdini ya risasi, sawa na utafiti wa mwaka 2015.
- Kiwango cha juu kabisa kilichoripotiwa ni kiwango cha vipande 84,000 kati ya vipande milioni moja ukilinganisha na vipande 99,000 kati ya vipande milioni moja kwa utafiti wa mwaka 2015.
- Hakuna kifungashio cha rangi zinazozalishwa Tanzania kinachotoa taarifa kwka mtumiaji kuhusu kiwango cha madini ya risasi kwenye rangi ama athari za madini ya risasi.

Shirika la Afya Duniani (WHO) limesisitiza kuwa madini ya risasi kwenye rangi ni janga la dunia kwa watoto ambalo lenye uwezekano mkubwa wa kuathiri afya zao hivyo kusisitiza kuwa "kutokana kuondolewa madini ya risasi kwenye petrol, madini ya risasi kwenye rangi ni chanzo kingine kikubwa hatarish kwa afya za watoto." Watoto wanaathiriwa na madini ya risasi kwnye rangi ikipakwa kwenye kuta na huchoka baada ya muda na hivyo kusababisha uuchafuzi wa makazi ndani ya yumba kama vumbi ndani ya nyumba na udingo. Watoto walio na umri kuanzia mwaka 0 mpaka miaka 6, wana tabia ya kueleka mikono yao kinywani mara kwa mara wapo kwenye hatari kubwa zaidi ya kupoteza uwezo wao kiakili na kukua ubongo kutokana na kuathiriwa na madini hayo yanayokuwamo kwenye vumbi na udongo. Ili kutatua tatizo hili la madini ya risasi kwenye rangi, AGENDA na IPEN wanapendekeza yafuatayo:

***Serikali na taasisi zake***

Utafiti umeonesha kuwa teknolojia za kuzalisha rangi zisizo na madini ya risasi zipo nchini ukizingatia rangi 25 kati ya 46 (asilimia 54 za rangi), ikiwamo zile zinazozalishwa nchini zimeonekana kuwa na viwango vya chini ya vipande 90 kati ya vipande milioni moja. Hivyo, shirika la viwango nchini (TBS) linahitajika kufanya haraka kusimamia kiwango cha 90 ppm cha madini ya risasi ya jumla kwa rangi zote za matumizi ya nyumbani za mafuta zinazozalishwa, zinazoagizwa toka nchi za nje, zinazosafirishwa kwenda nchi za nje, zinazosambazwa na kuuzwa kwa matumizi nchini Tanzania. TBS na ofisi ya mkemia mkuu (GCLA) ziyatake makampuni ya rangi nchini kuonesha viwango vya madini ya risasi katika maelezo ya kutosha katika vifungashio vya rangi yanayoonesha usumu wa madini ya risasi na viyeyushaji. Pia wakuze uelewa wa jamii kwa kufanya kampeni za madhara ya madini ya risasi pamoja hatua muhimu kupunguza athari za madini hayo.

***Wazalishaji wa rangi***

Baadhi ya makapuni ya rangi nchini bado yanazalisha rangi zenye mamdini ya risasi, hivyo basi waache mara moja kuzalisha rangi zenye madini ya risasi katika uzalishaji wake. Malighafi zisizo na madini ya risasi zipo nchini na zimekuwa zinatumiwa na baadhi ya makampuni nchini – rangi zilizoonekana kuwa na viwango chini ya 90ppm. Hakuna sababu ya msingi kwa wazalishaji kuendelela kuzalisha rangi zenye madini ya risasi nchini. Wanalazimika kuwajibika katika kulinda afya za jamii na mazingira kwa kuondoa uchafuzi katika hatua zote za rangi kama inavyoelekezwa katiaka xheria ya uzimamizi na uhifadhi wa mazingira ya mwaka 2004, Sehemu ya II, kifungu cha 4. Hatua hizi pia zinatakiwa kufuatwa kwa waagizaji na wasambazaji wa rangi nchini.

***Watumiaji wa Rangi (Mmoja mmoja, familia na taasisi)***

Watumiaji wa rangi wanahitajika kudai rang zisizokuwa na madini ya risasi toka kwa wazalishaji na wauzaji wa rangi pamoja na taarifa kamili za kilichomo kwenye rangi zao. Wanahitajika kuulizia, kununua wakiwa na uelewa na kupaka rangi zisizokuwa na madini ya risasi kwenye maeneo ambayo watoto wanapendelea kucheza kama vile nyumbani, shuleni, maeneo ya kupumzika na maeneo ya kuchezea. Taasisi lazima zipitie sera zao za manunuzi ili ijumuishe mahitaji ya rangi zisizo na madini ya risasi tu.

***Taasisi na makundi ya kitaaluma***

Makundi ya wataalamu wa afya, taaisis za watumiaji/walaji pamoja na taasisi nyinginezo zenye nia njema ziunge mkono juhud za kuondoa rangi zenye madini ya risasi na zianzishe shughuli za kuelimisha jamii kuhusu kulinda watoto kutokana na madini ya risasi kupitia rangi za nyumba, vumbi la madini ya risasi na udongo pamoja na vyanzo vingine.

***Wadau wote***

Wadau wote wanahitajika kwa pamoja kushirikiana ili kupigia upatu sera yenye nguvu ambayo itapelekea kuondoa madini ya risasi kwenye rangi Tanzania, sera itakayochangia mabadiliko katika manunuzi katika ngazo zote.

**Taarifa kwa wahariri**

Taarifa za utafiti huu zinazotolewa leo ni ya mwisho chini ya mradi wa kuondoa madini ya risasi katika rangi za nyumba ambapo mradi huu ulishirikisha wadau wa serikali, wazalishaji wa rangi na jamii kwa ujumla katika kujenga uwezo kuhusu athari zinazohusiana na madini ya risasi kwenye rangi. Mradi huu ulikuwa unatekelezwa katika nchi nne za Afrika (Tanzania, Caneroon, Ethiopia na Ivory Coast) chini ya ufadhili wa shirika la GEF (Global Environment Facility) la umoja wa mataifa Ulitekelezwa chini ya mwamvuli wa Shirika la umoja wa mataifa la mazingira (UNEP) na uliendeshwa na IPEN. Taasisi isiyo ya kiserikali ya AGENDA iliwajibika katika utekelezaji wa mradi nchini Tanzania. Mradi huu ulitekelezwa chini ya ufadhili wa GEF na shirika la mazingira la Umja wa Mataifa, uwajibikaji kwa maelezo ya taarifa hizi yapo chin ya AGENDA na IPEN tu. Si lazima GEF na shirika la mazingira la Umja wa Mataifa kuwa na mtizamo na tafsiri sawa za taarifa hii.

IPEN ni mtandao wa AZAKI 500 katika zaidi ya nchi 100 duniani zinazoshirikiana katika kutekeleza sera ya mazingira yasiyo na sumu kwa vizazi vijavyo na mshiriki wa kamitii ya ya ushauri ya mtandao wa kuonda madini ya risasi duniani (Global Alliance to Eliminate Lead Paint) mradi chini ya UNEP na WHO.

**- MWISHO -**

**Kwa taarifa zaidi**

Jina: Dorah Swai

Taasisi: AGENDA *for Environment and Responsible Development* (AGENDA)

Simu: +255 22 2461 052; +255 (0) 754 783 054

Barua pepe: swaidorah@yahoo.com ; agenda.environment1997@gmail.com

Anuani ya Skype: dorah.swai